



Atakaye hiji kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na hakufanya matendo mabaya, na hakufanya uwovu, atarudi kama siku aliyozaliwa na mama yake

Imepokelewa Kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Mwenyezi mungu ziwe juu yake- amesema: Nilimsikia Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- akisema: "Atakaye hiji kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na hakufanya matendo mabaya, na hakufanya uwovu, atarudi kama siku aliyozaliwa na mama yake"

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Anaweka wazi Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuwa atakaye hiji kwa kutaka radhi za Allah Mtukufu na akawa hakufanya yasiyofaa; Na yasiyofaa hapa maana yake ni tendo la ndoa na vitangulizi vyake, kama busu, kugusana, neno hili hutumika pia kumaanisha maneno machafu, na akawa hakufanya uovu; kwa kufanya maasi na madhambi, Na miongoni mwa uovu ni kufanya makatazo ya ihiramu (Hija), atarudi kutoka katika hija yake akiwa kasamehewa, kama azaliwavyo mtoto akiwa amesalimika kutokana na madhambi.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/2758>

